


# Wafugaji wafunzwe ufugaji wa kisasa

Baadhi ya wilaya zenye wafugaji wengi zimepoteza idadi kubwa ya mifugo baada ya kufa kutokana na ukame uliojitokeza uliosababisha ukosefu wa maji na malisho.

Kutokana na hali hiyo, mifugo 62,503 iliripotiwa kufa wilayani Simanjiro mkoani Manyara kwa kukosa maji na malisho katika vijiji mbalimbali.

Hiyo ni idadi ndogo ya kielelezo kuwa wafugaji wameshindwa kukabiliana na hali hiyo kwa sababu wana idadi kubwa ya mifugo ambayo imekuwa vigumu kuihudumia kwa kuwatafutia chakula.

Ukiacha Manyara, yapo maeneo mengine yaliyokumbwa na adha hiyo kama Morogoro, Tanga, Pwani.

Mifugo iliyopoteza uhai kwa kukosa malisho kwa mwaka uliopita siyo ng'ombe pekee, bali wapo kondoo, mbuzi na punda ambapo mifugo hiyo imekuwa na faida kwa anayefuga kwa kumpatia kipato baada ya kuuza.

Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara huenda ndiyo iliyopoteza mifugo mingi zaidi, kwani ng'ombe waliokufa walikuwa 35,746, kondoo 15,136, mbuzi 10,033 na punda 1,670.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega hivi karibuni aliwataka wafugaji nchini kuanza kuvuna mifugo yao na kuuza, kwani kwa kufanya hivyo kutawasaidia kuwaongezea kipato na kupunguza migogoro kati yao na watumiaji wengine wa ardhi.

Mbali na faida hiyo, kunasaidia mfugaji kujipunguzia hasara ya mifugo pale inapojitokeza janga kama la mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa mfugaji atakuwa na mifugo michache atakayoaweza kuihudumia nyakati za ukame kwa kuwatafutia malisho ya chakula eneo lililotengwa.

Pamoja na hayo, ni muhimu viongozi wa wilaya na wadau wa mifugo watengeneza mikakati ya kuhamasisha uvunaji wa mifugo kwa sababu somo la kupunguza mifugo, kunenepesha kwa kufuga kisasa, elimu hiyo bado inaonekana haijaeleweka kwa wafugaji wengi.

Baadhi ya wafugaji bado wana dhana kwamba kuwa na makundi makubwa ya mifugo ni ufahari, huku wakisahau kuwa kuna wakati hali hiyo kugeuka kuwa kero na kutopata faida endapo janga la aina hiyo litatokea.

Katika kuona umuhimu wa suala la ufugaji wenye tija, Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika bajeti ya mwaka 2021/2022 kuhusu uboreshaji wa huduma za mifugo imepanga kununua pikipiki 300 na kugawa kwa maofisa ugani nchi nzima, ili waweze kutoa huduma ya mifugo.

Mpango huo utaleta ahueni kwa kuwa maofisa hao wataweza kuwafikia wafugaji kila kona ya vijiji kuwapatia elimu mbalimbali kutokana na wengi wao kushinda zaidi maeneo ya mapori.

Maofisa ugani nchini waliopo ngazi za halmashauri za wilaya ni dhahiri sasa wataanza utaratibu wa kuhamasisha wafugaji kuanza uzalishaji na utunzaji wa vyakula vya mifugo na kutumia mvua zilizoanza kunyesha kuvuna nyasi na kuzitunza kwa ajili ya matumizi ya malisho wakati wa kiangazi.

Katika uhamasishaji huo, pia uwepo mpango wa kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi ya kipindi cha kiangazi kwa kuchimbwa malambo yatakayosaidia kupunguza adha na mateso wanayopitia wanyama wakati huo.

Hali ya kukua kwa uhitaji wa mifugo na mazao yake hapa nchini, nchi jirani na nchi za mbali kunatoa fursa ya kiuchumi kwa wananchi kujiongezea kipato kupitia mazao ya mifugo.

Umuhimu wa ufugaji unazidi kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya chakula na malighafi za viwanda, kwani sekta ya ufugaji

> **Pamoja na hayo, ni muhimu viongozi wa wilaya na wadau wa mifugo watengeneza mikakati ya kuhamasisha uvunaji wa mifugo kwa sababu somo la kupunguza mifugo, kunenepesha kwa kufuga kisasa, elimu hiyo bado inaonekana haijaeleweka kwa wafugaji wengi.**

ni muhimu kiuchumi kutokana na mchango katika Taifa, hivyo juhudi za kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wafugaji kufuga kisasa zinahitajika.

Mfugaji wa kisasa anahitaji kupata ushauri wa kitaalamu, hasa wa kuchagua ng'ombe wanaofaa kunenepeshwa kwa makundi yenye faida zaidi kwa nyama na maziwa kundi la zebu, Iringa red, Singida white wenye kuwa na uzito wa kilo kuanzia 200 hadi 300, wakati aina ya ankole wakianzia kilo 500 hadi 750 na boran wana uzito wa kuwa na kilo 500 hadi 1,000.

Benki ya NMB hivi karibuni ilitoa mafunzo ya unenepeshaji mifugo, ikiambatana na kauli mbiu ya 'Nenepesha upige pesa' kijiji cha Dakawa Mvomero kwa wafugaji wa Mkoa wa Morogoro, ili wafuge kibiashara na kuondoka katika ufugaji wa kizamani ambao hauna tija.

Mafunzo hayo yalitolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia mkufunzi, Dk Daniel Mdetele aliyeeleza faida za unenepeshaji ng'ombe kibiashara kuwa unampa faida mfugaji kuwalisha ng'ombe bila kuzurura kwa kuwapa chakula chenye protini, nguvu, vitamini na madini kwa muda usiozidi siku 90 na katika mazingira hayo humfanya ng'ombe kukua haraka na kuwa na nyama nzuri.

Scanned with CamScanner

wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wakikagua fremu za kuwekea biashara za mitumba, ...
wafanyabiashara wadogo maarufu machinga, Barabara ya Bahi, jijini humo jana.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

NIPASHE UK 15.

# Wafugaji wapewa sharti kumiliki mashamba

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka wafugaji kuhakikisha wanapima ardhi waliyonayo ili kupatiwa hati ya umiliki wa mashamba na kuepuka migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara.

Pia amewataka kuwa na ufugaji wenye tija kwa kufuga kisasa jambo litakalowasaidia kujikwamua kiuchumi wao na familia zao kupitia mifugo yao.

Mtaka aliyasema hayo jana, wakati akifungua mkutano kati ya wafugaji wa Mkoa wa Dodoma na viongozi wa mkoa, wenye lengo la kuwaelekeza juu ya umuhimu wa ushiriki wa sensa kwa wafugaji, pamoja na utambuzi wa mifugo.

Alisema ofisi yake itashirikiana na watu wa Idara ya Ardhi kutoa kipaumbele kwa wafugaji katika upimaji wa maeneo ili kuwa na hati miliki.

"Nakuelekeza mwenyekiti wa wafugaji nchini, waeleze wafugaji wako juu ya umuhimu wa kuwa na ardhi ambayo imepimwa, la sivyo wataendelea kusumbuka kila iitwapo leo kwa sababu ya kukwepa sheria ya umiliki ardhi," alisema Mtaka.

Alisema hivi sasa dunia inakwenda katika ufugaji wa kisasa wenye tija, hivyo ni vyema nao wakabadilika ili kuendana na wakati wa sasa, wapime mashamba yao ambayo yatawasaidia kutenga sehemu ya malisho ya mifugo.

"Ni wafugaji wachache sana ambao wana ng'ombe lakini hawana ardhi, hivyo hilo ni jambo la msingi, kuchukua hatua ya kupima ardhi mliokuwa nayo ili muwe salama," alisema Mtaka.

Alisema anahitaji kuona mfugaji anakuwa na bima ya afya, anasomesha watoto katika mazingira mazuri, anaishi sehemu nzuri kupitia ufugaji anaofanya.

Kuhusu uwekaji hereni kwenye ng'ombe, Mtaka alisema wafugaji wanapaswa kuondokana na dhana ya kupiga chapa ng'ombe kwa kutumia moto, badala yake wawavishe hereni ambazo zitawasaidia kufanya utambuzi wa mifugo waliokuwa nayo.

Alisema ng'ombe akiwekewa hereni hata akipotea ni rahisi kumpata kwa sababu tayari anakuwa kaingia katika mfumo wa utambuzi wa mifugo.

Alifafanua zaidi ya kuwa karne ya sasa kila kitu kwa mnyama kina thamani kuanzia ngozi ya ng'ombe hadi kwato zake.

"Jitahidini kuwavisha hereni mifugo yenu, itawasaidia kuitambua hata ikipotea kwenda sehemu nyingine," alisema Mtaka.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, aliwataka wafugaji kutumia elimu walioipata kuhusu ufugaji wa kisasa, ili kwenda kufanya mabadiliko ya ufugaji wanaofanya badala yake wafuge kwa tija.

Mfugaji kutoka Kongwa, Yared Yacob, aliushukuru uongozi wa mkoa kutokana na kuwapa elimu ya namna ya ufugaji wa kisasa, pamoja na kuwasisitiza kuvisha hereni mifugo ili kuwatambua kirahisi.

Scanned with CamScanner

MWANANCHI UK 13

## MTANIELEWA TU

Ofisa Mfawidhi Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji (Ruhila RABC) Nyanda za Juu Kusini Songea Ruvuma, Godfrey Maneno (wa pili kulia) akizungumza jambo kabla ya kuanza kushiriki mafunzo rejea kwa maofisa ugani wanaosimamia shughuli za ufugaji samaki mikoa ya Mbeya, Songwe, Ruvuma, Kigoma, Katavi na Rukwa. Picha na Joyce Joliga



Scanned with CamScanner

